Tuzungumze

Tufanyeje tunapoalikwa ?

Sheria ya kwanza ya kufwata unapoalikwa - nayo ni ya lazima sanani kuheshimia wakati. Fika kwa wakati na usicheleweshe wala kungojesha wenzako somo ao wale ambao waliokualika.

Huwezi kupima uzito wakitendo chako unapoalikwa kufika saa fulani na unafika saa moja baadae ! Katika wale walioalikwa pamoja nawe kunao wenyi madaraka mengi sana. Hawajui kungoja na pumziko lao ni kubadili vitendo. Kwao kupitisha saa nzima wakingoja na kungojea ni upotevu mkubwa wa wakati. Hujui kama kunao watu ambao dakika tanu, k.m., hutosha kwa kumiliki ma milioni ya pesa? Sasa ukimpotezea dakika zile si ni kumuuwa nusu?

Ni vibaya zaidi tena ikiwa ni wewe unayealika na hauheshimie saa uliyoandikisha wewe mwenyewe. Ni kukosa malezi kumwalika mtu mahali fulani, kwa wakati fulani ingawa unajua kama kwa wakati ule hautakuwa tayari mahali pale.

Utetezi wa mno si fadhila kwenyi mwaliko. Ukimya, lakini na unyamavu, vitakuheshimisha na kukulindia msafa.

Unapoenda mwalikoni jua kama watu watakutazama, hata wengine watakuchunguza wakiangalia wajue kama upo msafi, nguo gani umevaa, viatu, n.k..... ?

Kumbe kabla ya kutoka kwako fanya yote hata uwe katika hali ya kuonekana mbele za watu bila kosa: oga, chanua nywele zako, vika mavazi yako safi na nzima maana yake bila tundu wala mshonoko na yasiyokosa vifungo. Kwa aina ya vazi fuata ibada ya kila siku kuu au urafiki wako na wale waliokualika.

Ikiwa unayo desturi ya kutumia manukato fanya kwa ginsi manukato au marashi unayotumia isiwe ya harufu kali mno. Kunao watu wasiovumulia harufu ya marashi. Ukiwa jirani ya mtu wa aina ile na kama umepakaa marashi ya harufu kali mara utamchafua moyo jirani.

Mara nyingi uta... kwenyi uzazi, kweny... tanga; utaalikwa ... ikiwa ndugu, rafi... jirani amepata b... yupo msibani ama a... magumu fulani. Ku... pengine pote u... mwenyi maadibisho ... mwenendo wa adabu ... lekea kufurahisha ji... kuliko kujitafuta bi... si kujisahau kwa kuf... hisha jirani ndio ... ya maisha rasmi ka... ujamii.

(Na Kimengele Kimo...

MIAKA 20 YA MAPINDUZI YA ZAIRE

Ni mnamo tarehe 24 Novemba 1965 ndipo Mareshali Mobutu akishirikiana na maofisa wakuu alichukua madaraka ya uraïs wa Jamhuri.

Namna gani ?

Siku moja mbele apindue serikali, mheshimiwa Mobutu aliwakusanya maofisa wakuu wa askari. Na katika mkusanyo huo, maofisa hao walichungua kwa karibu ubovu na misukosuko ya siasa iliyokuwa yakisonga nchi. Na nchi ilikuwa ikiongozwa wakati huo na raïs Kasa-Vubu pamoja na waziri mkuu Tshombe Kapend. Katika masimulizi hayo muhimu, wakuu wa majeshi walichukua hatua ya kuangusha serikali na kuchukua madaraka bila kumwanga damu. Na hapo wakakubaliana yakuwa ni Mareshali Mobutu, wakati huo lietena-koloneli, ndiye atakuwa kiongozi wa Jamhuri ya Zaïre (hapo zamani Kongo).

Mnamo tarehe 24 Novemba 1965, asubui, kibarua toka maofisa wakuu kilifikia raïs Kasa-Vubu kikimjulisha kuwa hayupo tena raïs wa Jamhuri. Singa za simu zikakatwa na askari jeshi wakazunguuka vyumba kazaa vya serikali kama vile hivyo vya redio na Hoteli ya Posta. Punde kidogo wakuu na wakaaji wakaanza kusikia mziki wa askari jeshi na wa kimapinduzi.

Saa chache tu baada ya mapinduzi hayo kufanyika, habari hiyo ilitawanyika nchini kote toka sauti ya redio. Raia walipigwa na bumbuazi na wengi kurudi makwao kwa kungojea matokeo ya Mapinduzi. Nafasi zote, watu walikuwa wakinongonezeana na wakijiuliza kisa (but) kilichowasukuma maofisa wakuu hao wa askari kuchukua madaraka ya uongozi wa nchi.

Raïs Mobutu kwa Raïa

Siku tatu tu baada ya kuangushwa kwa raïs Kasa-Vubu pamoja na waziri wake mkuu Tshombe, mnamo tarehe 27 Novemba 1965, Raïs mpya wa Jamhuri, mwananchi Mobutu, aliwaelezea wapashaji wa habari kunako Jumba la Taifa (Palais de la Nation) kwamba atachukua madaraka muda wa miaka mitano.

Kisha mchana wa siku hiyo, raïs Mobutu aliwahotubia wakaaji wa mji wa Kinshasa ambao walifika wengi kwa kumsalimia kiongozi wao mpya. Siku hiyo Raïs Mobutu alijionya kwa raia uwanjani akisindikizwa na waziri wake mkuu, jemadari Mulamba Nyunyi wa Kadima na waziri wengine. Katika hotuba yake kwa Raïa, Raïs Mobutu aliwaelezea miradi (projets) ya kuimarisna uchumi wa nchi na siasa ya kidemokrasia ambayo wakaaji wote waliombwa kufuata.

Bisimwa L.-B. Tserou.

Raïs Mobutu pembeni ya akina mama Bobi Ladawa

Je Umesikia ?

KUWA feza zitafika kuwaunguza viongozi wa masomo ? Kutokana na pupa yake kali ya feza, kiongozi wa masomo ya sekondari ya pale Bagira (Institut de Bagira) alijiruhusu kuwashurtisha wanafunzi watoe nyongezo kwa feza za mchango wa wazazi ingawa liwali wa jimbo la Kivu amekwisha kuchukua mkataba juu ya jambo hilo. Kutokana na hesabu tulizofanya, yaonekana wazi kuwa wanafunzi wote watalipa kwa jumla zaïre 180.400. Feza hizo zote zaaminika kuingia katika mfuko wake. Lakini awe hakika kuwa wazazi wapo macho wazi. Na serikali haitakubali kumuacha huru mbele ya kosa hilo kubwa.

Yule wa masomo ya msinji ya Ibanda naye anakafilisha. Kamati ya wazazi nayo yaleta haya. Wanafia nini ? Feza. Haijulikani mpaka sasa feza zinazolipwa na wazazi zachukua njia gani. Kitu kilichoonyesha wazi kama mambo hayaendeki kule, ni kuona mkutano wa wazazi wa siku ya Mungu iliyopita unamalizika mbele ya wakati. Kumbe huko kiongozi pamoja na kamati ya wazazi watafuta kuwina nyuma ya migongo ya wananchi.

SHAHIRI

SAIDIA

Saidia ndugu, rafiki
Baba, mama, saidia !

Nisaidie dada kaka
Saidia maskini !

Mchana kutwa sikula
Sikunywa hata maji
Njaa na kiu hunisonga !

Ndugu nipe
Saidia Mungu
Atakurudishia milioni !

Fungua mkono
Leta pesa, franka
Bila wasiwasi !

Hauna kitu ?
Mungu akusaidie
Kesho unipe !

Nipe, nitalipa kish...
Hata kesho
Si bado nyuma !

Tangolek

PLASTI - ZAIRE

BUKAVU GOMA UVIRA KINSHASA

Musafiri mpenzi, pahali pa kupoteza ao kuponda pesa yako, pita peke yako "LA BOTTE", patana na PLASTI-ZAIRE upate kiatu ya kukuepusha popotopoto.

"PLASTI-ZAIRE": Kiatu yenyi kudumu inayopatikana ndani ya duka "PLASTI-ZAIRE" yapendeza watembezi wote.

"PLASTI-ZAIRE": Kiatu nzuri na nzito

"PLASTI-ZAIRE": Adui ajabu wa njia chafu

"PLASTI-ZAIRE": Kiatu ya kusaidia kusafiri bila uwasiwasi

"PLASTI-ZAIRE": Yakuletea utaratibu wa kutupa mguu na kuipatia hatua tamu

PLASTI-ZAIRE

BUKAVU GOMA UVIRA KINSHASA

PJ 264/P/85